

»Video za uzalishaji kutoka kwa Wadep: Asali«

Ufugaji wa nyuki ni mojawapo ya fursa za kibashara zenyefaida kubwa miongoni mwa wafugaji, kwani asali ni chanzo cha faida nyingi za kiafya na kimapato.

Kabla ya kuvuna asali mfugaji anatakiwa kuanda na kupanga vifaa vya kimsingi vinavyohitajika kama vile mavazi, kofia na barakoa, glovu za mikono, gumbooti, ḥendoo yenye mfuniko, kitao moshi, kisu na viberiti ili kuhakikisha usalama wakati wa kuvuna.

Shughuli za kabla ya kuvuna

Vaa nguo za kujikinga kila mara na hakikisha kwamba umelindwavya kutosha. Jaza kitao moshi na nyenzo za kutosha ambazo zitadumu katika kipindi cha kuvuna.

Washa kitao moshi na uvae mavazi ya kuvunia asali.

Shughuli za kuvuna

Puliza moshi kuanzia kando mwa mzinga, chini ya mfuniko na mlangoni ili kusababisha nyuki wanaozunguka mlango kurejea ndani ya mzinga.

Kisha ondoa mfuniko na upulize moshi ili kuhakikisha nyuki walioko juu ya mzinga wanaingia ndani. Tambua pande isiyio na asali, na kwa kutumia kisu gonga mbao za juu kwani masega matupu hufanya kelele kubwa zaidi.

Tumia kisu kuondoa mbao za juu ukianzia upande usio na masega. Pulizia moshi kwa nyuki zilizo kwa masega. Ondo nyuki kwa upole na uwaingize ndani ya mzinga. Kata masega yaliyokomaa na uyaweke ndani ya chombo.

Safisha pande za mbao za juu, zipange tena kama vile zilivyokuwa awali. Pulizia moshi kwenye juu yazo ili kuwafanya nyuki wote kuingia kwenye mzinga.

Usindikaji wa asali

Anza kwa kuvunja masega ukitumia kisu, yaweke kwenye kichungi safi, funika na kitambaa safi juu ya ndoo.

Funika chombo na mfuniko ili hewa isiingie. Hifadhi asali iliyochujwa kwenye vyombo vyatiki.